

MINUTE SHEETS

Dokezo No.

Kumb. Na. TAFIRI/HQ/W.I/Vol. IV/119

**WATUMISHI WOTE
TAFIRI**

Yah: **UWASILISHAJI WA MICHANGO YA PENSHENI KATIKA MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA (PSSSF) KWA WALIOKUWA WANACHAMA WA MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF)**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

1. Kutokana na maelekezo yaliyotolewa na Serikali pamoja na Chama cha Waajiri Tanzania (TAE), Waajiriwa katika Sekta ya Umma ambao walikuwa wanachangia katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii nchini (NSSF), watapaswa kuchangia katika Mfuko wa Pansheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Jumla ya mchango utakaowasilishwa ni asilimia 20 ukichangiwa kati ya mtumishi kukatwa katika mshahara (5%) na Mwajiri kumchangia pia (15%).
2. Uwasilishaji wa michango husika ulitakiwa kuanza tangu Mwezi Februari, 2019. Hivyo, michango iliyowasilishwa NSSF kuanzia Februari, 2019 itawasilishwa PSSSF.
3. Ikiwa kuna kipindi chochote ambacho mtumishi anadaiwa na NSSF kuanzia mwezi Januari 2019 kurudi nyuma, michango husika itapaswa kulipwa NSSF. Hivyo, mnshauriwa kuangalia "contribution summary report" ili kujiridhisha kuwa hakuna michango ambayo haikuwasilishwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2019 kurudi nyuma. Aidha, miezi iliyochangiwa katika Mfuko wa NSSF italindwa kisheria wakati wa kulipa mafao ya watumishi husika.

MINUTE SHEETS


Dokezo No.

4. Watumishi wote waliokuwa wanachangia katika Mfuko wa NSSF wanatakiwa kujaza fomu za Uanachama za Mfuko wa PSSF (Member Registration Form). Kwa watumishi waliopo Makao Makuu na Kituo cha Dar es Salaam, fomu zinapatikana katika Ofisi ya Masjala (Makao Makuu) na kwa wale wa Vituoni (Mwanza, Kyela, Kigoma) na kituo kidogo cha Sota, fomu zinapatikana kwa HRAOs/Watumishi wanaotekeleza majukumu ya HRAOs.
5. Kwa watumishi wa Makao Makuu na Kituo cha Dar es Salaam, fomu zilizojazwa kikamilifu ziwasilishwe Masjala. Kwa watumishi wa Kituo cha Kigoma, Kyela na Kituo Kidogo cha Sota fomu zilizojazwa kikamilifu zitumwe Makao Makuu, Dar es Salaam kwa ajili ya taratibu nyingine. Na wale wa Kituo cha Mwanza, fomu husika zikabidhiwe kwa HRAO.

6. Zoezi hili likamilika kabla ya tarehe 19 Agosti, 2019.

(Majina ya waliokuwa wanachama wa NSSF yameambatishwa)

Nawatakia kazi njema.



Joan J. Ndibalema

SHRAO

05/08/2019

Nakala: Ag. DG (aione kwenye jalada)

